



BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

MABORESHO YA MFUMO WA KIELEKTRONIKI WA KUSAJILI MIRADI YA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA (TAM)

Mnamo mwaka 2020 Baraza liliimarisha miundo mbinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usajili wa miradi ya TAM ambao ulianza kutumika mwezi Oktoba 2020 kwa kusajili Miradi ya Tathmini za Mazingira na Ukaguzi (*Online Registration and Tracking System*). Mfumo huu unawawezesha wawekezaji kusajili miradi yao na kufuatilia mchakato wa Hati ya Mazingira kielektroniki (*Online*).

Mfumo huu unatumiwa na makundi yafuatayo:

- i. Waandaaji wa Miradi kusajili mradi;
- ii. Watumishi wa Baraza kupokea na kufanyia kazi maombi yanayowasilishwa ya TAM; na
- iii. Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) kufanyia kazi maombi ya TAM kabla ya Waziri kuidhinisha utekelezaji wa miradi.

Katika kuboresha huduma hii, mfumo huu umeboreshwa kwa kuongeza wigo wa makundi ya miradi na huduma nyingine kama ifuatavyo:

- i. Miradi ya barabara na miundombinu ya umeme (*linear projects*);
- ii. Miradi ya minara ya mawasiliano (*Communication Towers projects*);
- iii. Maombi ya Kibali cha Muda cha Kufanya Maandalizi ya Awali ya Mradi (*Provisional Environmental Clearance - PEC*);
- iv. Maombi ya kufanya mabadiliko kwenye cheti cha awali (*Variation*);
- v. Maombi ya kuhamisha umiliki wa mradi na cheti cha mazingira (*Transfer*), na;
- vi. Maombi ya kuacha kabisa kutekeleza mradi (*Surrender*).

Maboresho haya ni katika jitihada zinazofanywa na Baraza za kuendelea kutekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha mazingira bora na wezeshi kwa wawekezaji hususan walio na lengo la kuanzisha shughuli za maendeleo.

Mfumo huu unapatikana kwenye tovuti za Baraza kutokana na kundi husika kama ilivyoainishwa hapa chini:

- i. Waandaaji wa Miradi (*eia.nemc.or.tz*);
- ii. Watumishi wa Baraza (*pms.nemc.or.tz*); na
- iii. Watumishi katika Ofisi ya Makamu wa Rais (*vpo.nemc.or.tz*).

Kwa misingi hiyo, taasisi zote nchini, wawekezaji, wataalam elekezi, wananchi na wadau wote wa mazingira mnataarifiwa kuwa usajili wa miradi ya makundi yaliyotajwa hapo juu pamoja na maombi ya Kibali cha muda (*PEC*), *Transfer*, *Variation* na *Surrender* vimeanza kufanyika kwa mfumo wa kielektroniki. Kuanzia tarehe 1 Julai 2021 Baraza halitapokea maombi ya miradi na vibali vilivyotajwa yatakayowasilishwa kwa njia ya nakala ngumu.

Kwa taarifa zaidi tembelea tovuti ya Baraza (*nemc.or.tz*) au tembelea Ofisi za Makao Makuu ya Baraza zilizopo katika Kiwanja Na. 28-30, Mtaa wa Regent, Mikocheni au katika ofisi za kanda za Baraza zilizopo Arusha, Dodoma, Kigoma, Mbeya, Mtwara na Mwanza.

Limetolewa na:

***MKURUGENZI MKUU,
BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)***

Limesambazwa na:

***Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma, Baraza la Taifa la
Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), S.L.P 63154, Dar es Salaam.
Simu: +255 22 2774889, +255 22 2774852 na 0713 608930/ 0692108566,
Barua pepe: dg@nemc.or.tz***